

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

**KUSITISHA KWA MUDA LESENI YA HUDUMA YA
UTANGAZAJI WA MAUDHUI MTANDAONI YA
JAMBO ONLINE TV**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inatoa taarifa kwa Umma kuwa, mnamo tarehe 31 Machi, 2026, Jambo Online TV kupitia akaunti yake ya utangazaji wa maudhui mtandaoni ya Instagram pamoja na chaneli yake ya utangazaji wa maudhui mtandaoni ya Youtube ilichapisha maudhui ambayo hawakuwa na uhakika nayo na yasiyo na uthibitisho. Maudhui hayo pia yaliupotosha umma kuhusu hali ya matukio mbalimbali yanayoendelea nchini na matokeo yanayotarajiwa kutoka kwa Tume ya kuchunguza matukio wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, kinyume na Kanuni za Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020 na Marekebisho yake ya mwaka 2022 na 2025.

Aidha, katika kipindi kifupi cha takribani miezi sita sasa, yaani tangu mwezi Septemba, 2025, Jambo Online TV imekuwa na mashauri manne (4) mfululizo ya ukiukaji wa Sheria, Kanuni, Masharti ya Leseni, Maadili, Misingi na Taaluma ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

Hivyo basi, kwa mujibu wa Kifungu cha 114 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura 306 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023, TCRA INASITISHA kwa muda wa **Siku Tisini (90)**, kuanzia tarehe 02 Aprili, 2026, Leseni ya Maudhui Mtandaoni iliyotolewa kwa Jambo Online TV ikiwa ni pamoja na kusitisha utoaji wa huduma ya utangazaji wa maudhui mtandaoni ya Jambo Online TV katika chaneli na akaunti zake zote za mtandaoni.

Imetolewa tarehe **02 Aprili, 2026.**

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU